

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA



**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU KUREJESHA KWA HUDUMA YA  
MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA  
NA WATU WENYE ULEMAVU.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya **Geita** anawatangazia wananchi juu ya urejeshwaji wa Huduma ya Mikopo inayotolewa kwa Vikundi vya wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu. Mikopo hii imerejeshwa Rasmi kuanzia tarehe 27/08/2024.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo Hii baada ya kurejeshwa vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri,
- (ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,
- (iii) Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo Timu ya Menejimenti

ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye Ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,

- (iv) Kikundi kiwe na **akaunti ya benki** iliyofunguliwa kwa **jina la kikundi** kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
- (v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka **18** na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka **18 hadi 45**.

Aidha baada ya kurejeshwa kwa mikopo hii na kutajwa kwa makundi yanayostahili kupata mikopo hii, Halmashauri inaendelea na maandalizi mengine ya utoaji wa mikopo hii. Wananchi wote mnatangaziwa kufika kwenye ofisi za kata au Halmashauri kwaajili ya kuendelea kupata taarifa Zaidi za mikopo hii. Mnaweza pia kutembelea website ya Halmashauri ambayo ni [www.geitadc.go.tz](http://www.geitadc.go.tz)

**Tangazo hili limetolewa na: -**

**Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Geita**



**Karia R Magaro**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**GEITA**

